# GRETSA UNIVERSITY - THIKA

## UNIVERSITY EXAMINATIONS

## SEPT-DEC 2016 SEMESTER

## CERTIFICATE IN EARLY CHILDHOOD EDUCATION

**COURSE CODE: CECE 010**

**COURSE TITLE: KISWAHILI**

**TAREHE:** **SAA: 3**

**INSTRUCTIONS TO CANDIDATES**

1. SEHEMU YA KWANZA **A**: NI YA **LAZIMA**
2. SEHEMU YA PILI **B**: JIBU MASWALI YOYOTE **MATATU**
3. **USIANDIKE CHOCHOTE** KWENYE KARATASI YA MTIHANI. KWA KUFANYA HIVYO UTAKUWA UMEVUNJA SHERIA ZA MITIHANI NA UTAADHIBIWA
4. ANDIKA VIDOKEZO VYAKO **NYUMA YA KIJITABU CHA MAJIBU** KISHA PIGIA MSTARI BAADAYE

***TAHADHARI***:- *kamera za CCTV zipo kwenye vyumba vyote vya mitihani*

**SEHEMU YA A: NI YA LAZIMA (Alama 40)**

1 A i) Ufahamu: Soma kifungu kifuatacho kasha ujibu maswali. (Alama 15)

Nchi ya Keny inasifika kote duniani kutokana na hali nzuri ya hewa. Nchi hii hupatikana katika ukanda wa Ikweta. Jua hupatikana kwa mwaka mzima. Hali hii nzuri ya hewa huwavutia watalii chungu nzima kutoka kila pembe ya dunia. La kushangaza ni kuwa, hali ya hewa hutofautiana sana kutoka sehemu moja ya nchi hadi nyingine. Ukienda Nyanja za juu na maeneo ya milimakama vile mlima Kenya, utapata hali ya baridi . kileleni mwa mlima Kenya kuna hata theluji.

Uteremkapo kuelekea Mwambao wa Pwani, viwango vya joto huwa juu kutokana na bahari Hindi. Maeneo ya ziwa Viktoria pia hupata viwano vya juu vya joto. Mbali na hali nzuri ya hewa, ipo misitu iliyojaa wanyama pori wa kila aina na miti ya kila aina. Kadhalika kuna mbuga na hifadhi za wanyama. Hili huwa ni vutio kubwa sana watalii. Aidha, kuna mito iliyo na mianguko ya maji. Mfano mzuri ni mwanguko wa Thompson na mianguko ya Thika na Chania.

Kunazo chemichemi za maji moto katika Bonde la Ufabazo huwaacha watalii vinywa wazi. Isisahaulike kuwa ni katika mkao uo huo Mwanya Mkuu ambapo ipo milima ya ajabau kama vile Menengei ambao una kreta kileleni. Kutokana na mvuo ya kutosha, mazao mengi hukuzwa katika sehemu nyingi za nchi. Mimea hiyo ni kama vile, mipareto, mpunga, mipamba,michai, mikademia nikitaja tu michache.

Yapo pia madini kama vile mgadi huko Magadi,chokaa n.k. je wajua nchi hii ina misimu minee katika mwaka?

a) Toa mada/kichwa mwafaka kwa kifungu ulichosoma.(al.2)
b) Taja makli asali yaliyotajwa katika kifungu hiki. (Al. 5)
c) Orodhesha mbuga tatu za wanyama pori nchini Kenya(Al.3)
d) Ni zipi hifadhi nne za wanyama nchini Kenya? (Al.4)

ii) Andika barua rasmi ukiombA kazi ya ualimu katika shule ya chekechea ya ‘Staha Academy’(Al.10)

iii) Taja huku ukitoa mifano aina za nomino unazofahamu. (Al.10)

iv) weka maneno yafuatayo katika kauli ya kutenda. (Al.5)

a)Shuka

b)Imba

c) Soma

d)Andika

e)Chora

1 B) Andika katika wingi. (Al.5)

i. Sufuria -
ii. Kijiko-
iii. Chumba-
iv. Njia-
v. Wimbo-

C) Toa kinyume cha maneno haya: (Al.5)

i. Muumini
ii. Mjomba
iii. Mbingu
iv. Umoja
v. Mume

D) Tungs sentesi zozote tano kwa kutumia msamiati wa mahakamani, ujenzi na nafaka. (Al. 10)

E) Weka sentensi hizo katika hali ya wingi (Al.10)

F) Andika maneno matano katika ngeli ya‘A-WA’. (Al.10)

| Mfano katika Umoja | uwingi |
|---|---|
| Mtoto | watoto |

G) Kamilisha methali zifuatazo. (Al.5)

i. Chelewachelewa………………………………………………………………………
ii. Mtaka cha mvunguni…………………………………………………………………

iii. Samaki mkunje………………………………………………………………………
iv. Asiyesikia la mkuu……………………………………………………………………
v. Subira……………………………………………………………………………………..

H) Taja tanakali za Sauti unazojua. (Al.5)

I) Tungs sentensi kwa kutumiaa maneno yafuatayo. (Al.5)

Daktari

Saa

Wivu

Ulemavu

Masomo

J) Andika sentensi zifuatazo katika:

I. Msemo wa taarifa

i. “Njoo hapa wewe!” Mama alimwita. (Al. 2)
ii. Weka mezani hicho kikombe” Shukri alimweleza Amina. (Al.2)

K) Weka sentensi ifuatayo katika wakati ujao(Al.1)

i. Alimwona na kumwita

L) tofautisha kimaana maneno haya tatu. (Al.10)

i. Karamu na Kalamu
ii. Shuka na suka
iii. Ghali na kali
iv. Somea na zomea
v. Linda na rinda

M) Tambua vitenzi nomino katika sentensi hizi. (Al.10)

i. Mama anapika pilua
ii. Kake yake huendesha gari moshi
iii. Mjomba alileta ngombe wetu
iv. Kipchoge ni mkimbiaji hodari
v. "Andika kwa kalamu ya wino" Mwalimu alimwambia Amina.

**SEHEMU YA B: JIBU MASUALI YOYOTE MATATU (Alama 60)**

2 a) "Lugha ni kwa ajili ya mawasiliano pekee" Toa maoni yako kwa kikamilifu huku

ukipinga au kukubaliana na tamko hili. (Alama 10)

b) Je, lugha ya binadamu hutofautiana vipi na lugha ya wanyama? Sanisi utungo huu.

(Alama 10)

3a) Angazia kwa kikamilifu uhusiano uliopo baina ya Isimu na Lugha. (Alama 10)

b) Tathmini tofauti iliopo kati ya stadi ya maandishi na ile ya mazungumzo kwa kuonyesha

utofauti huo kwa mujibu wa sifa kuu na mifno mwafaka. (Alama 10)

4a)"Kila kitu huwa na chanzo chake na hakichipuki tu kutokana na ombwe tupu!"Sanisi

kauli hii kwa mujibu wa lugha. (Alama 15)

b) Jadili historia y Isimu kwa kurejelea Isimu katika karne ya ishirini. (Alama 5)

5a)Umepewa fursa ya kumfasilia mtu asiyelewa dhana ya lugha. Toa maelezo

yako kwa kuzingatia mada hizi:

i) Tabia za lugha (Alama 10)

ii) Sifa kuu zalugha (Alama 10)

6a) Tathmini aina za lugha huku ukitolea mifano kwa mujibu wa jamii pana

ya nchi ya

Kenya. (Alama 10)

b) Tathmini tofauti kati ya Kirioli na Pijini. (Alama 4)

c) Utatambua vipi iwapo mzungumzaji wa lugha fulani ni mzawa wa lugha hiyo? (Alama 6)